BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** sifa zote anastahiki Mwenyezi Mungu aliyetuumba, kutujaalia uhai na uzima uliotuwezesha kupata fursa hii adhimu na muhimu ya kukutana katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa kwa lengo la kutekeleza jukumu letu la msingi lililoelezwa katika Kifungu cha 88(b) cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 kuhusiana na miongoni mwa kazi kuu ya Baraza la Wawakilishi ya kupitisha Bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kueleza hotuba ya Kamati ya PAC, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza vyema Baraza hili kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu. Aidha, nathamini juhudi zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi za kuhakikisha anazingatia misingi ya Utawala Bora katika Serikali anayoiongoza hususan kwa kufuata utawala wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Nitakuwa sijatenda haki, ikiwa nitaacha kumshukuru Kiongozi wa Shughuli za Baraza ambae pia ni Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah kwa kusimamia ipasavyo majukumu ya Wizara zote za Serikali ambapo Zanzibar na wananchi wetu wanamatumaini makubwa ya kunufaika na utekelezaji wa Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa uwasilishaji ulio tukuka pamoja na jitihada zake anazozichukua za kusimamia utendaji na Watendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hususan kwa kuhakikisha anahudhuria ipasavyo katika vikao vyote vya Kamati licha ya kuwa na majukumu mengi yanayomkabili. Sambamba na hilo, tunawashukuru Watendaji wa Afisi ya CAG akiwemo Mdhibiti na Naibu Mdhibiti wa Afisi hiyo pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Mdhibiti kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kuchambua na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Hata hivyo, Kamati yetu iliendelea kufanyakazi siku ya tarehe 5 na tarehe 9 Mei, 2025 kwa kukutana na Watendaji wa Idara ya Bajeti pamoja na kuziita Taasisi zenye Madeni ya miaka iliyopita ya Ada za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya Kudumu ya 119(1), Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la Mwaka 2024) pamoja na mambo mengine, Kamati ya PAC inalo jukumu la kujadili bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kulitekeleza jukumu hilo, Kamati yetu ilikutana na Watendaji wa Afisi hiyo siku ya Jumatano ya tarehe 30 Aprili, 2025 kwa ajili ya kujadili pamoja na kuchambua utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025 na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 322,400,000 kama Mapato ya ndani. Hata hivyo, hadi kufikia Machi, 2025, imeweza kukusanya jumla ya shilingi 108,772,900 sawa na asilimia 33.73 ya makadirio hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imebaini kuwa tofauti kubwa iliyopo kati ya Makadirio na Mapato halisi yaliyopatikana ilitokana na matokeo ya makadirio yasiyokuwa na uhalisia ambayo kimsingi yanaratibiwa na kupangwa na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango bila ya kuzingatia hali halisi ya uwezo wa Afisi ya CAG katika ukusanyaji wa mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii imeendelea kujirudia kwa miaka kadhaa mfululizo ambapo Afisi ya CAG haijawahi kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato yaliyopangwa kwa takriban miaka mitano iliyopita, jambo ambalo linaipelekea Afisi hii kuonekana ina mapungufu ya ukusanyaji wa mapato katika vitabu vyake hali ya kuwa udhaifu huo unatokana na upangaji wa bajeti bila kuzingatia tathmini sahihi ya uwezo wa mapato kwa taasisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu ilifanya tathmini ndogo juu ya sababu zinazopelekea Afisi ya CAG kushindwa kufikia lengo la makusanyo iliyopangiwa kwa kuangalia Toleo la Orodha ya Taasisi ambazo zinapaswa kutozwa Ada ya Ukaguzi iliyotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango la mwaka 2021, Kamati ya PAC ilibaini kuwa orodha hiyo ni ya muda mrefu tangu kutolewa kwake na imeshapitwa na wakati kwa vile viwango vilivyomo ndani yake havilingani na hali halisi iliyopo.

**Mheshimiwa Spika,** viwango vilivyoainishwa kutozwa Ada ya Ukaguzi katika Toleo la Orodha hiyo ni shilingi 17,600,000 kwa Taasisi zenye uwezo mkubwa wa kifedha kama vile Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mamlaka ya Mapato Zanzibar, shilingi 8,800,000 na shilingi 7,000,000 kwa Taasisi zenye uwezo wa kati na kati zikiwemo Mamlaka ya Usafiri Baharini, Shirika la Nyumba na Shirika la Utangazaji Zanzibar wakati shilingi 6,000,000 zinatozwa kwa Taasisi zenye uwezo mdogo kama vile Kampuni ya Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia viwango hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya Taasisi zinatozwa Ada ndogo ukilinganisha na mapato halisi ya Taasisi hizo. Kwa msingi huo, Kamati yetu imeiagiza Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kufanya tathmini

itakayowezesha kutambua uwezo halisi wa makusanyo kwa Taasisi zinazotozwa Ada ya Ukaguzi na Afisi ya CAG na hatimae kuvifanyia mapitio viwango vinavyoendelea kutumika ili Wizara iweze kuja na viwango vipya ambavyo vitaendana na wakati tulionao na uwezo halisi wa Taasisi zinazotozwa ada hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaamini kuwa kufanya hivyo kutaiwezesha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuinua uwezo wake wa kukusanya mapato zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu pia imebaini kwamba uwezo wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufikia malengo ya ukusanyaji wa Shilingi 500,000,000 ni mdogo sana kutokana na uhalisia kwamba hata Taasisi zote zikilipa Ada ya Ukaguzi hawataweza kufikia hata nusu ya fedha za makadirio hasa ukizingatia hadi mwezi wa Machi, 2025 Afisi hiyo imekusanya asilimia 33.73 ya makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujua kwanini Afisi hii imeongezewa makusanyo kwa zaidi ya shilingi 177,600,000 wakati makusanyo aliyopangiwa awali hakuweza kuyafikia. Sambamba na hilo, Kamati ilihoji kwanini kuwepo na ongezeko la makusanyo wakati wigo (scope) ya kazi ya Afisi ya CAG itapungua katika mwaka 2025/2026 kutokana na harakati za Uchaguzi Mkuu wa 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba kuna Taasisi ambazo awali zilikuwa zikipewa ruzuku na CAG alikuwa hakusanyi Ada ya Ukaguzi kwao lakini hivi sasa zimeachiwa kuwa ni Taasisi zinazojitegemea. Hivyo, CAG ataruhusiwa kuongeza mapato yake kupitia Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC haikuishia hapo ilitaka kujua Taasisi hizo ni ngapi na zipi na kuelezwa kwamba Taasisi hizo zipo saba ambazo ni Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA), Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji (ZIPA), Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Mamlaka ya Mji Mkongwe, Taasisi ya Viwango (ZBS) na Kamisheni ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia ukweli wa majibu hayo, Kamati yetu ilibaini kuwa ni Taasisi mbili tu kati ya hizo ambazo ni Taasisi ya Viwango (ZBS) na Kamisheni ya Ardhi ambazo hazikuwemo katika Toleo la Mwaka 2021. Mbali na hilo kuna Taasisi ambazo zimo katika Toleo hilo lakini kwasasa zimeshaunganishwa ama kufutwa ikiwemo Kampuni ya Ujenzi ambayo itapunguza mapato yaliyokusudiwa kupatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa msingi huo, uwezekano wa Afisi ya CAG kufikia malengo ya makusanyo yake siku zote utabakia kuwa ndoto isiyotekelezeka na hali hiyo itakuwa inaathiri ufanisi wa Afisi hiyo (Revenue collection performance) kwa kuonekana haifanyi vizuri katika Taarifa zake za hesabu wakati kiuhalisia sio sahihi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa madeni ambayo Afisi ya CAG inazidai Taasisi za

Serikali Ada ya Ukaguzi, Kamati yetu imebaini kuwa kuna Taasisi za Serikali zinadaiwa takribani shilingi 178,200,000 ambazo ni fedha zinazotokana na malimbukizo ya madeni yaliyokuwa hayajalipwa kwa zaidi ya mwaka mmoja baada ya ukaguzi kufanyika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kulitafutia ufumbuzi suala hili, Kamati ya PAC iliziandikia barua ya wito Taasisi zote zinazodaiwa ili kushiriki kikao kilichofanyika tarehe 9 Mei, 2025 ambacho pamoja na mambo mengine, Kamati yetu ilibaini yafuatayo:

1. Taasisi zinazodaiwa hazijashirikishwa katika uandaaji wa Toleo la Orodha ya Taasisi na kiwango kinachotakiwa kulipa Ada za Ukaguzi. Hali hiyo imepelekea baadhi ya Taasisi kulalamika kwamba zinapangiwa viwango vya malipo ya Ada za Ukaguzi kinyume na uwezo walionao.
2. Miongoni mwa sababu za Taasisi husika kulipa Ada ya Ukaguzi ni kwamba Taasisi husika iwe na sifa ya Taasisi inayojitegemea. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kimaumbile kuna Taasisi kweli zinazo sifa hizo lakini kiuhalisia katika utendaji wake bado hazijitegemei kikamilifu. Kwa msingi huo hutegemea fedha za Matumizi Mengineyo wanazopatiwa kulipa Ada ya Ukaguzi na baadhi ya wakati hushindwa kufanya malipo kutokana na upungufu au ukosefu wa fedha.
3. Baadhi ya Taasisi huwa hazipangi bajeti ya kulipa Ada ya Ukaguzi. Hali hiyo imepelekea kushindwa kuwa na kifungu ambacho fedha hizo zinatakiwa kuombewa na kulipwa badala yake hutumia fedha za shughuli nyengine. Kamati inaziagiza Taasisi zinazostahiki kulipa Ada ya Ukaguzi kupanga mapema katika bajeti zao ili kuhakikisha utekelezwaji wake.
4. Baadhi ya Taasisi hufanya malipo ya Ada ya Ukaguzi lakini malipo hayo hushindwa kuonekana katika kumbukumbu za hesabu ya Afisi ya CAG kutokana na changamoto ya kimtandao. Aidha, kuna baadhi ya Taasisi huonekana kuwa hazijafanya malipo kutokana na kukosea kuziandika kwa usahihi ‘control number’. Hili limethibitishwa na Kamati yetu kwa kuangalia vielelezo vya malipo ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar.
5. Baadhi ya Taasisi za Serikali zimekuwa na Viongozi wapya na Taasisi nyengine vielelezo vya maombi havijapatikana kutoka na sababu tofauti na kupelekea kutokuwa na taarifa ya kudaiwa deni lililopita. Hali hiyo imepelekea kulipa Ada ya Ukaguzi kulingana na wakati husika. Kwa msingi huo, Kamati inaiagiza Afisi ya CAG kuwasilisha barua ya ukumbusho wa madeni inayodai (debt remind letters) kwa Taasisi zote inazozidai hususan Shirika la Nyumba (ZHC), Bodi ya Usajili Wasarifu na Wakadiriaji Majengo na Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA).
6. Baadhi ya Taasisi zilipeleka maombi ya kusaidiwa kulipwa deni hilo Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Serikali. Hata hivyo, Kamati yetu ilibaini maombi hayo yalikuwa nje ya muda ambao yalistahiki kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa hatua za malipo. Barua yenye kumbukumbu nambari ZBC/MD/2021/VOL.1/79 ya tarehe 22/4/2024 inahusika. Hivyo, Kamati imeliagiza Shirika la Utangazaji Zanzibar lilipe deni hilo la shilingi 7,000,000 la mwaka 2021/2022.
7. Baadhi ya Taasisi hizo zimefanikiwa kulipa deni hilo katika mwezi huu wa Mei,

2025. Taasisi hizo ni Wakala wa Ulinzi wa JKU shilingi 7,000,000, Mamlaka ya Usafiri Baharini na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Aidha, Bodi ya Usajili Wasarifu na Wakadiriaji Majengo imepanga kulipa deni lake katika mwezi huu wa Mei, 2025.

8. Baadhi ya Taasisi hukaguliwa Kitaifa na Kimataifa na hulipa madeni yao kwa wakati lakini huwa hawapatiwi Taarifa iliyokaguliwa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka (Audited Financial Report). Kutokupatiwa taarifa hiyo hupelekea changamoto wanapokaguliwa Kimataifa au wanapotaka kutumia taarifa hizo kwa shughuli zao za kiutendaji. Changamoto hiyo inaikabili Mamlaka ya Usafiri Baharini. Hivyo, Afisi ya CAG ihakikishe inazifanyia kazi na kuzipatia Taasisi hizo kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kutoa barua za kuziita Taasisi zinazodaiwa, Hata hivyo, kuna Taasisi za Serikali zilishindwa kuitikia wito huo bila ya kutoa sababu yoyote ya msingi. Miongoni mwa Taasisi hizo ni Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) shilingi 35,200,000, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) shilingi 8,800,000, Kampuni ya Uvuvi Zanzibar shilingi 18,000,000 pamoja na Kampuni ya Ujenzi shilingi 17,600,000.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana kutokushiriki kwao, Kamati imepata wasiwasi kwamba ama Taasisi hizo huwa hazitaki kwa makusudi kulipa au hudharau kazi inayotekelezwa na Afisi ya Mkaguzi. Hivyo, Kamati itaendelea kulifuatilia deni ambalo linadaiwa Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 2,244,700,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi 2025, Afisi hiyo imefanikiwa kupata jumla ya shilingi 1,531,292,000 sawa na asilimia 68.2% ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kushindwa kupata asilimia 100 ya fedha za Matumizi Mengineyo, Kamati ya PAC ilihoji ni kwa namna gani Afisi hiyo imeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ikiwemo kutoa mafunzo kwa Watendaji wake ili kuweza kufanya ukaguzi na kuyafikia maeneo yote kwa ajili ya ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu ilibaini kwamba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipanga kukagua Miradi ya Kimkakati ya Maendeleo 30, lakini kutokana na uhaba wa fedha za matumizi mengineyo (OC), Afisi hiyo iliweza kukagua Miradi 20 tu ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi wa miradi hiyo ni muhimu sana kutokana na ukweli kwamba fedha nyingi za Serikali zimewekezwa kwa lengo la kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar. Hivyo, umma utashindwa kujua changamoto zilizopo na hatimae kuwajibishwa wale wote wanaobainika kuhusishwa na kadhia ya utekelezaji mbaya wa Miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaiomba Serikali kuiangalia kwa jicho la huruma Afisi

hii kwa kuipatia fedha za kutosha zitakazowezesha utekelezaji wenye ufanisi wa kazi za ukaguzi kwa maslahi ya Wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhishwa na utekelezaji wa Bajeti ya Afisi hii kama ilivyoainishwa katika Fungu E04 la Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Kadhalika, Kamati yetu inaipongeza Afisi ya CAG kwa kuweza kufungua Maabara ya Ukaguzi wa Kiuchunguzi "forensic Audit Lab" ambayo sasa itaiongezea uwezo Afisi ya CAG kufanya ukaguzi wa kitaalamu na ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mafunzo kwa Watendaji wake, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetumia njia mbali mbali ikiwemo matumizi ya fedha za OC, ushirikiano wa ufadhili mbali mbali ikiwemo mradi wa PFMRP na BSAAT pamoja na ushirikiano wao baina ya Afisi ya CAG Zanzibar pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania (NAOT). Kamati yetu inaisisitiza Afisi ya CAG kuhakikisha inaendelea kuwapatia mafunzo Watendaji wake ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya ukaguzi yanayotokea ulimwenguni.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza maoni haya yanayohusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaliyoandaliwa na Wajumbe wa Kamati yetu. Kwa umuhimu wa kipekee, na kwa ruhusa yako, naomba sasa nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe na Makatibu wa Kamati yetu kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma Ali Khatib | - | Mwenyekiti; |
| 2. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | - | M/Mwenyekiti; |
| 3. | Mhe. Abdalla Hussein Kombo | - | Mjumbe; |
| 4. | Mhe. Kombo Mwinyi Shehe | - | Mjumbe; |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | - | Mjumbe; |
| 6. | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Mjumbe; |
| 7. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | - | Mjumbe; |
| 8. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu; |
| 9. | Ndg. Adam Maulid Simai | - | Katibu; |
| 10. | Ndg. Fatma Omar Ali | - | Katibu; |
| 11. | Ndg. Maryam Haji Ali | - | Katibu; |

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine, naomba kuchukua nafasi hii kutamka kuwa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) imeyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/2026. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muipitishe ili ile mipango mizuri iliyopangwa na Afisi hii iweze kutelekelezwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja kwa asilimia 100 naomba kuwasilisha.

……………………
Mhe. Juma Ali Khatib,
Mwenyekiti,
Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC),
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**